



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, S.L.P. 28, Mtaa wa Chamaguha, Shinyanga.  
Simu:028-2763213, Barua pepe: md@shinyangamc.go.tz, tovuti: [www.shinyangamc.go.tz](http://www.shinyangamc.go.tz)

Unapojibu tafadhali taja

Kumb. Na SHY/MC/S.20/47 VOL I

Tarehe:21/02/2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI YA MAKAZI NA  
POSTIKODI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga anapenda kuwatangazia wananchi wote nafasi za ajira ya muda kwa nafasi za wakusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi katika kata na mitaa yote ya Manispaa ya Shinyanga.

**A. SIFA ZA MUOMBAJI**

- i. Awe Raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka **18 – 40**
- ii. Awe na Elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea
- iii. Awe anamiliki simu janja yenye uwezo wa kukaa na chaji siku nzima
- iv. Awe na barua pepe inayofanya kazi
- v. Awe ana uwezo wa kusoma ramani za mitaa
- vi. Awe ni mkazi wa kata husika

**B. KAZI NA MAJUKUMU**

- i. Kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- ii. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- iii. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa anwani za makazi.
- iv. Kutuma Taarifa ya mfumo wa Anwani za Makazi katika Kompyuta kuu
- v. Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku **30**.

**C. VIAMBATISHO**

Maombi yaambatishwe na:

- i. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea.
- ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- iii. Paspoti size mbili (2)
- iv. Barua ya maombi ipitie kwa mtendaji wa mtaa na kata anapoishi


**D. JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya muombaji, namba ya simu na barua pepe ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga kwa anwani ifuatayo:

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA,  
MANISPAA YA SHINYANGA,  
S.L.P 28,  
SHINYANGA.**

**E. TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **25/02/2022** saa **9:30** Alasiri.

  
Jomaary M. Satura  
**MKURUGENZI WA MANISPAA**  
MKURUGENZI WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA  
SHINYANGA